CCM Ole yaridhishwa ujenzi wa chama

FATMA SULEIMAN, PEMBA

CHAMA cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Kusini Pemba, kimetoa pongezi kwa juhudi ambazo amezionesha mwakilishi wa jimbo la Ole, Masoud Ali Moh'd, za kukijenga Chama sambamba na kuwaletea maendeleo endelevu wananchi wa jimbo hilo.

Akizungumza Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi (CCM)mkoa wa Kusini Pemba, Yusuf Ali Juma, alisema jimbo la Ole limekitendea haki chama kwa kumchagua mwakilishi mwenye kuumwa na shida za wananchi.

Kwa upande wake Katibu wa CCM mkoa wa Kusini Pemba, Kajoro Peter Vyohoroka na Katibu wa siasa na uenezi Mkoa wa Kusini Pemba, Fat-hia Hemed Saidi, walisema katika kukiboresha Chama, Mwakilishi huyo amejenga na kuboresha Ofisi zote za Chama ndani ya jimbo hilo, ikiwa ni katika kutekeleza ahadi alizoziweka kwa wananchi hivyo ni vyema kuyaenzi yale mazuri walioletewa na mwakilishi wao.

"Yaenzini matunda ambayo mumeyapata kupitia Mwakilishi wenu kwani nimengi amewafanyia kwenye Jimbo hili", alisema.

Nae, Mwenyekiti wa Jimbo la Ole, Hassan Abdallah Ali, alieleza zaidi ya miaka 20 hawakuwahi kuona mafanikio ambayo wameyapata hivyo wataendelea kuzienzi juhudi zilizochukuliwa na mwakilishi za kuwaletea mabadiliko ndani ya jimbo hilo.

Alisema Mwakilishi huyo amekuwa akileta maendeleo bila ya kubagua chama chochote hivyo aliwaomba na viongozi wengine kuiga mfano wake ili kuendelea kuleta mabadiliko .

Aliwataka wananchi wa Pemba kutokufanya makosa na kuchagua viongozi wenye mfano wa Massoud katika kuwaletea maendeleo na kuleta mabadiliko katika sekta zote ikiwemo ya kielimu Afya ,miundombinu ya barabara maji na hata Umeme .

"Nawaomba wananchi tuchaguweni mfano wa Massoud ili tuweze kupata Maendeleo kwa haraka zaidi,"alisema.

Katika hafla hiyo matawi matano ambayo aliyajenga kuanzia foundation hadi juu amekabidhi TV na vingamuzi kila tawi pamoja na viti vya kukalia.

Micheweni yafunguka kiuchumi - Shamata

NA MWANTANGA AME

WAZIRI wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo, Shamata Shaame Khamis, amesema Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Mwinyi, anastahili pongezi kubwa kwa kazi yake aliyoifanya ya kukinua maendeleo kisiwa cha Pemba, kutokana na kutekeleza vyema ilani ya Uchaguzi.

Waziri huyo aliyasema hayo katika ukumbi wa Baraza la Wawakilishi huko Chukwani nje kidogo ya Mji wa Zanzibar, wakati akichangia hotuba ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi.

Waziri huyo alisema, Dk. Mwinyi anastahili pongezi hizo kwani ameonesha kwa vitendo kutekeleza ilani hiyo kivitendo katika sekta mbali mbali ikiwemo ya barabara na kilimo.

Alisema hapo awali serikali ilikuwa ikijenga barabara kupitia miradi ya kilimo ukiwemo MIVA lakini zilikuwa ni za kifusi ambazo hazikudumu kutokana na mvua ikinyesha zinaondoka, jambo ambalo wakulima walikuwa wakizilalamikia.

Alisema hali hiyo imekuwa ikiwafanya wakulima kushindwa kufikisha mazao yao kwa wakati katika masoko na wakati mwengine mazao hayo kuharibika, jambo ambalo limekuwa likiwasababishia kupoteza nguvu zao.

"Nakubaliana na tukubaliane sote kwa pamoja kwamba yalopangwa kutekelezwa yametekelezwa kwa vitendo maana nchi hii tumekaa kwa miaka mingi sana dhamira ya serikali awamu kwa awamu ilikuwa nzuri sana na kupata ufanisi lakini kwa mwaka huu tumeshuhudia kila anaesimama hakuna jimbo ambalo hakuna miradi mikubwa iliyoachwa Mimi nataka kutoa ushuhuda kwa Michweni" alisema Waziri huyo.

"Kwa niaba ya wananchi wa Micheweni tunataka kutoa shukrani zetu kwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Mwinyi, sisi tumejengewa Bandari, na Bandari hii yetu sote Zanzibar nzima lakini sisi tutafaidika zaidi na Bandari hii".

Waziri huyo alisema uchumi wa Watu wa Micheweni umeanza kufunguka kama dhamira aliyokusudia Dk. Mwinyi ya kukifungua kiuchumi kisiwa cha Pemba.

Alisema hiyo ni kutokana na kufanya ujenzi wa barabara huku akiamua kupeleka shilingi bilioni 5. 772, 506, ambazo zimetumika kwa ajili ya ujenzi wa bandari ya Shumba Mjini kwa awamu ya kwanza.

"Hali ya Micheweni imebadilika katika kipindi kifupi sana sasa hivi hata wale wafanyabiashara wa samaki na fanyabiashara wa shughuli nyengine sasa hivi Micheweni ni jambo la kawaida kumekuwa ni karibu mno wakati miaka ya nyuma kulikuwa kunaonekana ni mbali nah ii imetupa hamasa na kuona sasa tumeambiwa na serikali kwamba tutaletewa meli zinauwezo wa kubeba tani 2000 zitaweza kushusha maeneo ya Shumba Mjini" alisema Waziri huyo.

Alisema wale wanaohisi wananchi wa Micheweni wamewahishwa kupelekewa maendeleo, waone ukweli huo kwani walicheleweshewa lakini sasa wameanza kuona mafanikio yake.

Alisema ujenzi wa barabara katika Jimbo hilo wanaishukuru serikali kwani Dk. Mwinyi, alisema atazifungua kwa pamoja na hivi sasa wananchi wanafaidi matunda yake kwani kutoka Micheweni kwenda Shumba Mjini barabara zina lami.

Alisema inafurahisha serikali inakusudia kujenga barabara maalum kwa ajili ya gari zinazobeba mizigo kutoka katika Bandari hiyo, pamoja na barabara ya kutoka Kiuyu kwenda Maziwa ng'ombe zimejengwa nyingi pamoja na maeneo mengine ikiwemo Finya Kicha, Mapofu Tumbe, na Konde Msuka.

Makontena 317 yashushwa bandari ya Mkoani

NA MWANTANGA AME

NAIBU Waziri wa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Nadir Abdulatif, amesema tangu serikali kumpa muwekezaji Bandari ya Mkoani tayari meli 13 na makontena 317 yameweza kuhudumiwa kupitia bandari ya Mkoani kwa kipindi cha miezi sita.

Naibu huyo aliyasema hayo, wakati akijibu suala la Mwakilishi wa Kiwani kisiwani Pemba, Mussa Foum Mussa, aliyehoji mafanikio gani yaliyopatikana hadi sasa na Je, ni meli ngapi za makontena zimeingia nchini kupitia bandari ya Mkoani tangu alipokabidhiwa muekezaji.

"Tunaipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Shirika lake la Bandari, kwa kufanikiwa kutumika bandari ya Mkoani katika kupokea meli za makontena na kukabidhi bandari hiyo kwa mwekezaji husika" alisema.

Naibu Waziri huyo, alisema tangu mwekezaji huyo apewe kuiendesha Bandari hiyo tayari Meli 13, na makontena 317 yameweza kuhudumiwa kupitia bandari ya Mkoani kwa kipindi cha miezi sita.

Kutokana na hatua hiyo alisema mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na kurahisisha upakiaji na ushushaji wa bidhaa kama vile karafuu na mwani, kuongeza ajira kwa vijana katika kuhudumia makontena kupitia ICD ya Mkoani pamoja na gharama za upakiaji wa mizigo.

Wizara inapokea pongezi kwa kufanikisha matengenezo ya Gati ya Mkoani Pemba kwa kuiwezesha kupokea meli za makontena.

ADILI AUCTION MART LIMITED

Court Brokers, District Land and Housing Tribunal Brokers, Debt Collectors, Auctioneers, Real Estate Agents & General Trading

TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

MAHAKAMA YA MWANZO WILAYA YA SONGWE

KITUO CHA MWAMBANI

SHAURI LA MADAI NA.15/2025

MASAGA NGWESA .... **MDAI**

DHIDI YA

LEHA NDIZU.. **MDAIWA**

KWA IDHINI TULIYOPEWA NA **MAHAKAMA YA MWANZO MWAMBANI**, TUTAUZA KWA MNADA WA HADHARA NGOMBE 19 WALI**OPO** ENEO LA GUA WILAYA YA SONGWE MKOA WA SONGWE. MNADA UTAFANYIKA TAREHE 09/06/2025 SAA 7:30 MCHANA.

MASHARTI YA MNADA

1. NGOMBE WATAUZWA KAMA WAILIVYO
2. MNUNUZI ATAKAYE SHINDA ATALIPA MALIPO YA AWALI YA 25% YA BEI ITAKAYOFIKIWA SIKU YA MNADA NA 75% KATIKA MUDA WA SIKU 14.
3. MNUNUZI ATAKAYESHINDWA KUMALIZIA SALIO LA 75% KATIKA MUDA ULIOPANGWA HAPO JUU HATARUDISHIWA FEDHA ALIZOLIPA AWALI NA MNADA UTARUDIWA SIKU NYINGINE ITAKAYOPANGWA
4. GHARAMA ZOTE ZA USAF**IRISHAJI**, NA GHARAMA NYINGINEZO ZITAKUWA JUU YA MNUNUZI

MAWASILIANO

HEAD OFFICE: PLOT NO 151 BLOCK 45C KIJITONYAMA MAKUMBUSHO AREA DAR ES SALAAM BRANCH OFFICE VWAWA MBOZI DISTRICT SONGWE

TEL: 0686585630/0693298296

E-MAIL: info@adiliauction@.co.tz /nkkmvungi@gmail.com